

UFUTUHI: SILAHA YA JADI ILIYOTUMIWA NA SHAABAN ROBERT KUPAMBANA NA UKOLONI

Athumani S. Ponera

Chuo Kikuu cha Dodoma
athuman.ponera@udom.ac.tz

Ikisiri

Makala hii inabainisha namna mbinu ya ufutuhi ilivyotumika kama silaha ya kijadi ya kupambana na ukoloni. Utafiti uliozalisha makala hii ulitumia Nadharia ya Uhemnitiki. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbili, usaili na uchambuzi wa matini, kisha kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Inabainishwa katika makala hii kuwa riwaya ya Kusadikika ni shambulizi kali lililolekezwa kwa wakoloni, ambapo Shaaban Robert anabeua na kuing'ong'a mifumo ya kikoloni. Aidha, anaizindua jamii kuhusu umuhimu wa kujipapatua kutoka kwenye mikatale ya kikoloni. Kutokana na miktadha mbalimbali ya kikoloni iliyokuwa inamzunguka, aliweza kupenyeza shambulizi kwa maadui zake kwa kutumia aina nne za ufutuhi: ufutuhi wa majazi, ufutuhi wa balagha, ufutuhi wa unyume, na ufutuhi wa utanakuzi. Makala inahitimisha kwa kuwahamasisha waandishi ambao ni miongoni mwa makundi yanayotegemewa zaidi na jamii katika kuiongoza, kuikosoa, na kuiokomboa, kuendelea kuvaa ujasiri wa kufanya kazi yao kwa kutumia mbinu anuwai.

Dhana za Msingi: Ufutuhi, Ujadi, Ukoloni.

1.0 Utangulizi

Katika makala hii, ufutuhi unajadiliwa kama mojawapo ya mbinu za kibunilizi ambazo waandishi huzitumia ili kusana kazi zao. Ufutuhi, chambilecho Ponera (2014), unatumiwa kama dhana inayoweza kuzaa matokeo ya tabasamu, kicheko, furaha, na ucheshi. Attardo (2001) na Billig (2005) wanaongeza kuwa ufutuhi hutokana na maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye mnato na mvuto. Kwa kawaida, maneno, matendo, au matukio yenye uwezo wa kuzua ufutuhi hubebwa kupitia vijenzi kama vile kejeli, dhihaka, stihizai, ufyosi, ubeuzi, tashtiti na utani.

Kwa mujibu wa Ponera (2014), zifuatazo ni baadhi ya sifa za ufutuhi. Mosi, ni dhana jumuishi ambayo hufumbata vijenzi mbalimbali vyenye uwezo wa kutoa matokeo yanayolandana. Vijenzi hivyo ni kama vile kejeli, dhahaka, ubeuzi, stihizai, tashtiti, ufyosi na utani. Matokeo yake ni tabasamu, kicheko, furaha, na ucheshi. Pili, ufutuhi hufungamanishwa na mwanadamu; yaani huundwa, kutolewa, na kuelekezwa kwa mwanadamu. Tatu, huweza kudhihirishwa kwa kutumia maumbo kama vile maneno ya mdomo, maandishi, matendo, vibonzo au picha tuli. Nne, ni dhana inayoambukiza. Ufutuhi ni jambo litokealo katika mazingira ya kuwapo kwa watu wengi kuliko mazingira ya upweke. Tano, hutawaliwa na dhana ya ‘kusahau’ masuala mengine yanayoumiza au kusongamana akilini. Sita, ufutuhi siyo suala la kinasibu, bali ni la kikanuni. Billig (2005) anaeleza kuwa ufutuhi hutokea kwa mpokezi kutokana na ama ridhiko la nafsi (kutokana na mvuto wa kinachowasilishwa) au kuwapo kwa msigano baina ya uhalisi wa kitu kinachowasilishwa na namna kinavyowasilishwa.

Kwa mujibu wa Ross (1998), ufutuhi ni dhana inayotegemea sana misingi ya kipokezi. Hivyo, hadhira huweza kutofautiana katika kuuibua katika matini hiyo hiyo moja. Ross (ameshatajwa) anaongezea kuwa ufutuhi huweza kujitokeza katika matini ya kifasihi kwa uwazi au kwa ufiche. Ufutuhi fiche husanwa kwa kutumia jazanda za kiwango cha juu. Hivyo, huhitaji upeo wa juu na muda wa kutosha ili hadhira aweze kuubaini. Attardo (2001) anabainisha kuwa, miongoni mwa vigezo vinavyoleta tofauti katika kuuibua ufutuhi ni: uhusiano wa kijamii kwa wale wanaofanyiana ufutuhi (kama vile umri na kazi wafanyayo), hifadhi ya maarifa, miktadha inayounganisha hadhira na suala linalowasilishwa, pamoja na idili¹ za kijamii. Ufutuhi ni nyenzo inayotumiwa na kila jamii katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Vilevile, kila jamii huunda na kutumia ufutuhi kulingana na idili zake. Hali hii huufanya ufutuhi kuwa dhana yenye mwegamo wa kijadi. Dhana ya ujadi inatumiwa katika makala hii kumaanisha vipengele vya kiasili vinavyojitokeza katika matini ya fasihi (Shitemi, 2008). Hivyo, ufutuhi unajadiliwa kama jambo la kiasili.

¹ Idili ni nguzo au misingi inayoaminiwa na jamii kama kipimo cha ubora au utendekaji wa mambo, Idili huibuliwa na jamii husika.

Shaaban Robert ni miongoni mwa waandishi wanaoutambulisha uandishi wa zama za urasimi mkongwe wa fasihi ya Kiswahili (Madumulla, 2009). Kipindi cha uandishi wake (kuanzia miaka ya 1930 hadi 1960) kiligubikwa na tawala za wageni katika nchi ya Tanganyika. Kezilahabi (1976) anasisitiza kuwa, kutokana na kuwapo kwa watawala hao wa kigeni, hapakuwa na uhuru uliowaruhusu waandishi kusawiri mazonge mengi yaliyokuwa yanajiri kwa Waafrika. Hivyo, yamkini, zilihitaika mbinu na silaha maridhawa kwa kila mwanajamii ili kupambana na madhila hayo. Waandishi ni kundi mojawapo la jamii. Nao walitakiwa kubungua bongo ili wafanikiwe kuandika na kuchapisha kazi zao, hususani zilizohusu ukoloni. Hivyo, kila mtunzi alitumia mbinu na silaha aliyoimudu.

Shabaha ya makala hii ni kuonesha jinsi Shaaban Robert alivyotumia mbinu ya ufutuhi katika kupambana na wakoloni. Mjadala wa namna alivyopambana na wakoloni unafanywa kwa kuegemezwa katika riwaya yake ya *Kusadikika*. Hoja inayojengwa hapa ni kuwa, riwaya hii ni shambulizi kali kwa wakoloni ambalo liliviringishiwa ufutuhi.

2.0 Nadharia Iliyotumika

Makala hii ni zao la utafiti ulioongozwa na Nadharia ya Uhemnitiki. Kwa mujibu wa Newton (1997), Uhemnitiki ni taaluma inayohusiana na kutafsiri maana ya matini, hususani matini zenye misingi ya kihistoria, kifalifa na kiteolojia. Nadharia hii iliasisiwa na Friedrich Schleiemacher. Kisha, iliendelezwa na Martin Heidegger na Wilhem Dilthey (Eagleton, 1996). Wamitila (2002) anaongeza kuwa Nadharia ya Uhemnitiki inaamini kwamba maisha ya binadamu huathiriwa kwa njia mbalimbali na asasi, mifumo, na miktadha tofauti inayomzunguka. Wadau wa nadharia hii wanaamini kuwa, hata muda mrefu kiasi gani ukipita, maana inayotokana na matini huwa haibadiliki. Hali hii husababishwa na mabadiliko ya mitazamo ya wahakiki wa matini hiyo. Kuwapo kwa matini zinazotakiwa kuendelea kutumiwa na vizazi mbalimbali vinavyoendelea kutokea ulimwenguni kunazalisha haja ya kuwapo kwa nadharia kama hii ya Uhemnitiki inayohusiana na njia au mbinu za uelewaji wa maana za matini.

Mhimili mkuu unaoshikilia nadharia hii ni Duara ya Kihemnitiki. Hii ni dhana jumuiifu inayosisitiza kuwa, uelewaji wa maana ya matini huhusisha kuyafahamu mambo mbalimbali

yaliyomzunguka mtunzi wakati au kabla ya kuitunga matini husika (Newton, ameshatajwa). Mhimili huu mkuu unafumbata mihimili mingine ambayo ni ufufuaji na utukuzaji.

Ebeling (1964) anaeleza kuwa, kwa muktadha wa Nadharia ya Uhemnitiki, utukuzaji humaanisha makisio ambayo msomaji au mhakiki wa kazi ya fasihi huwa nayo aanzapo kuisoma kazi hiyo. Makisio hayo hujengwa akilini mwa msomaji kwa kutumia tajriba binafsi, anwani ya kazi, kiwango cha usomi, utamaduni, upeo wa uelewa, pamoja na ulinganisho wa kazi zozote zilizotungwa na watunzi wengine zinazofanana na hiyo. Kuhusu ufufuaji, Eagleton (1996) anafafanua kuwa ni uhuishaji wa uhalisi uliokuwepo wakati au kabla ya kuzaliwa kwa matini. Muasisi wa mhimili huu, Dilthey, anasisitiza umuhimu wa mhakiki au msomaji kufufua muktadha asilia wa kazi inayohusika kwa kujaribu kujiweka katika muktadha huo ili aweze kuipata maana asilia ya matini (Wamitila, 2002).

Kwa pamoja, mihimili hii ya utukuzaji na ufufuaji ambayo inafumbatwa na mhimili mkuu, Duara ya Kihemnitiki, inategemea sana dhana nyingine ya ‘hifadhi ya maarifa’. Dhana hii, chambilecho Attardo (2001), hujumuisha kumbukumbu mbalimbali zinazohusiana na matini husika. Kumbukumbu hizo ndiyo msingi wa kufanikiwa kwa Duara ya Kihemnitiki, yaani ukisiaji na uhuishaji. Kwa muktadha wa kiini cha makala hii inayohusu matumizi ya ufutuhi kama silaha ya kijadi ya mapambano dhidi ya ukoloni, dhana hii ya hifadhi ya maarifa tunaitumia kama mhimili unaojitegemea. Hivyo, kwa jumla, imetumika misingi mitatu ambayo ni utukuzaji, ukisiaji, na hifadhi ya maarifa.

Katika kupata maana ya matini iliyotafitiwa (riwaya ya *Kusadikika*), nadharia hii imetumiwa kwa kuzingatia hatua nne. Mosi, riwaya teule ilisomwa kwa kina ili kutafuta kuwapo kwa ushikamani wa matukio hayo ili kupata maana kuu. Pili, tulitumia fikra zetu binafsi kukisia maana za jumla zinazotokana na viashiria vya jumla katika riwaya teule kama vile anwani, majina ya wahusika, lugha iliyotumika, na maudhui yanayosawiriwa. Tatu, tulitumia hifadhi ya maarifa kutafakari na kuchanganua hali halisi ya kijiografia, kiutamaduni, kisiasa, kisanaa, na kihistoria, ya kabla au wakati mtunzi anaandika riwaya teule. Hatua hii ya kutumia hifadhi ya maarifa, chambilecho Attardo (ameshatajwa), ni kiunganishi cha kukisia na kuhuisha hali halisi ya miktadha iliyopita. Kwa hiyo, hatua hii ndiyo iliyotupatia mwanga zaidi wa kuweza

kuhusisha matukio mbalimbali yaliyomo riwayani na vipengele vingine vya kimaisha. Vilevile, tulivihusisha viashiria hivyo na tabia halisi ya mwandishi mwenyewe. Nne, tulitumia maarifa yaliyopatikana kutokana na hatua ya kwanza hadi ya tatu hapo juu kupata maana ya matukio hayo.

3.0 Jinsi Ufutuhi Ulivyotumika kama Silaha katika Riwaya ya *Kusadikika*

Sehemu hii inawasilisha matukio yenye maudhui yanayoshambulia ukoloni kwa kutumia ‘silaha’ ya ufutuhi. Kabla ya kusawiri matukio hayo, yanatolewa maelezo mafupi kuhusu riwaya ya *Kusadikika*.

3.1 Maelezo Mafupi kuhusu Riwaya ya *Kusadikika*

Riwaya ya *Kusadikika* ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1948. Toleo linalotumiwa katika makala hii ni la mwaka 1951. Suala linalojichomoza zaidi katika riwaya hii iliyojengwa kidhahania ni elimu ya sheria. Robert aliamua kutumia suala hili kama nguzo ya usimulizi wa vitushi vya riwaya hii kwa sababu ya hali halisi ya maisha ya wakati huo wa kutungwa kwake. Kazi hii iliandikwa wakati Tanganyika (sasa ni Tanzania) ikiwa inatawaliwa na Waingereza. Utawala huo wa kikoloni ulikuwa unawaonea wananchi wa Tanganyika. Waafrika hawakuwa huru kupanga na kuamua juu ya mambo mbalimbali kuhusu maisha yao. Mifumo muhimu ya maisha yao ilipangwa, kutekelezwa, na kuamuliwa na wakoloni; hivyo, kusababisha waishi kwa kubinywa katika nyuga mbalimbali za maisha.

Miktadha hiyo ya kikoloni ndiyo iliyomuibua Robert kuonesha hisia za masikitiko kupitia kazi zake. Katika riwaya ya *Kusadikika*, anawasilisha hisia hizo kupitia kesi iliyomkabili Karama ambaye ni mhusika mkuu. Kesi hiyo inabainisha suala la kupuuzwa kwa matunda ya safari zilizofanywa na wajumbe wa nchi ya Kusadikika katika nchi nyingine. Kutokana na hali hiyo, anaibuka Karama ambaye anagundua kuwa watu wa Kusadikika wapo katika lindi hilo la mazonge kutoka kwa watawala wao kutokana na kukosa elimu. Anaamua kuanzisha darasa la kuwapa Wasadikika elimu ya sheria ili wajikwamue. Kitendo hiki ndicho kinachomfanya Karama akabiliane na mashtaka ya uchochezi na uhaini. Masimulizi ya utetezi wa Karama juu ya mashtaka haya ndiyo yajengayo vitushi vikuu vya riwaya ya *Kusadikika*.

3.2 Ufafanuzi wa Matukio ya Kifutuhi katika Riwaya ya *Kusadikika*

Ufutuhi aliyotumia Robert katika riwaya hii uko katika makundi manne. Nayo ni: ufutuhi wa majazi, ufutuhi wa balagha, ufutuhi wa unyume, na ufutuhi wa utanakuzi.

3.2.1 Matukio ya Ufutuhi wa Majazi

Kwa mujibu wa TUKI (2004), majazi ni jina ambalo mtu, kitu au mahali hupewa ili kuelezea hali, sifa, tabia, mwonekano au dhima yake. Katika uga wa fasihi, usawiri wa wahusika wa kimajazi ni mtindo wa kuwapa wahusika wa kazi ya fasihi majina yenye maana maalumu inayodokeza na kuwasilisha sifa na tabia ya mtajwa kwa namna ya mafumbo. Kuna majazi yenye uwezo wa kuibua ufutuhi na yale yasiyo na uwezo huo.

Kusadikika ni riwaya iliyosheheni matumizi ya majazi (ya kawaida na yale yenye uwezo wa kuibua ufutuhi). Majazi katika riwaya hii yanaonekana kupitia vipengele vitatu. Kipengele cha kwanza ni jina la kazi yenyewe (*Kusadikika*). Kipengele cha pili ni ujenzi wa dhamira zake (kama vile ‘u-jeta’ unaomaanisha uvivu, ambao kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), miongoni mwa maana za neno ‘jeta’ ni ‘mtu mvivu apendaye kuwatuma wenzake wamletee vitu hata kama viko karibu naye’; ‘kufanya maringo kwa kitu ulichonacho; na kujivuna). Kipengele cha tatu ni ujenzi wa wahusika wake. Majina ambayo Shaaban Robert ameyatumia kimajazi katika *Kusadikika* ni Karama pamoja na wajumbe sita waliojitolea kwenda kusaka elimu na ujuzi katika nchi mbalimbali zinazopakana na nchi ya Kusadikika. Wajumbe hao ni: Auni, Fadhili, Kabuli, Buruhani, Ridhaa na Amini. Majina mengine ya kimajazi ni yale ya viongozi wa Kusadikika kama yanavyotambulishwa na Majivuno, Waziri Mkuu wa nchi hiyo, wakati anasoma mashtaka ya Karama. Nayo ni: “Bwana Taadabuni, Katibu wa Serikali, Bwana Komeni, Amiri Jeshi, Bwana Fujo, Mlinda Hazina, Bwana Boramimi, Mudir wa Sheria” (uk. 5).

Kila mmoja kati ya wahusika hao amepewa uwezo na dhima inayoakisi jina lake. Jina la Kusadikika linatokana na kitenzi ‘sadiki’ kinachomaanisha kuamini. Mtunzi amewasawiri wananchi wa Kusadikika wakiwa na sifa ya kuamini. *Karama* ambaye jina lake linamaanisha kipawa, katika riwaya hii anajitokeza na kutumia vipawa vyake vya “...ubongo wa hekima, moyo wa ushujaa na ulimi wa ufasaha” (uk. 8) ambavyo amejaaliwa katika kuwakomboa wajumbe sita,

yeye mwenyewe, na Wasadikika wote. *Majivuno* ni sifa inayoelezea hali ya kujitukuza, kujiona na kujisifu. *Fujo* ni ghasia au kukosekana kwa mpangilio wa mambo au utulivu. *Taadabuni* linatokana na neno adabu au heshima. Kutaadabu ni kuadabisha au kutia adabu. *Komeni* linatokana na kitenzi ‘koma’ chenye maana ya acha. *Boramimi* linamaanisha sifa ya ubinafsi na kujipendelea.

Kwa upande wa majina ya wajumbe sita, *Fadhili* lina maana ya kutoa msaada au mambo mema. Katika kazi hii, Fadhili amejitolea kuwafanyia fadhila watu wote wa Kusadikika. *Auni* maana yake msaada. Katika riwaya teule, Auni anajitokeza kuwasaidia Wasadikika. *Kabuli* lina maana ya kuafiki na kukubali. Katika riwaya hii, Kabuli, licha ya kuyajua madhila yaliyowafika watangulizi wake, akakubali kubeba dhima ya kwenda katika nchi ya Kusini kusaka maarifa. *Buruhani* maana yake kipaji kutoka kwa Mungu. Buruhani wa nchi hii ya Kusadikika pia alijaaliwa kipaji maalumu ambacho alikitumia katika kuikomboa nchi yake. *Ridhaa* ni ridhiko au hiyari. Mjumbe huyu aliridhishwa na dhima aliyopewa; na, kwa hiyari yake, alijitolea kuikomboa nchi ya Kusadikika. *Amini* maana yake sadiki. Amini naye aliyaamini mawazo yake pamoja na uwezo wake. Pia, aliamini kwamba kujitolea na kujijusurisha kwake ndio msingi wa ukombozi wa nchi yake.

Katika makala hii, tunayafafanua baadhi ya majina yaliyotumika kifutuhi. Jina la nchi ndilo linaloanza kutufunulia dhana ya ufutuhi. Mtunzi ameitambulisha kazi yake kwa kuiita ‘Kusadikika - Nchi Iliyo Angani’. Katika utangulizi, anazidi kuifafanua nchi hiyo anaposema:

Kusadikika ni nchi ambayo kuwako kwake hufikirika kwa mawazo tu. Nchi hiyo iko katikati ya mipaka sita. Kwa upande wa Kaskazini imepakana na upepo wa Kaskazi, na kwa upande wa Kusini imepakana na upepo wa Kusi. Mashariki imepakana na Matlai, na Magharibi mpaka wake ni upepo wa Umande. Kwa kuwa nchi yenyewe inaelea katika hewa kama wingu, zaidi ya kupakana na pepo nne hizo, ina mipaka mingine miwili, mipaka miwili yenyewe ni hii: Kwa juu nchi hiyo imepakana na Mbingu, na kwa chini imepakana na Ardhi (uk.vii).

Katika tukio hili ndipo ufutuhi unapoanzia. Mandhari hiyo ya nchi ya Kusadikika pamoja na maelezo ya mipaka yake yapo nje ya uhalisi. Aghalabu, hali hii huweza kuzua ucheshi msomaji anapojikita katika maana yake ya msingi, ambayo inamfanya mtu aione nchi hii ikielea angani. Ucheshi huo unaweza kutokea kutokana na ukinzani wa kifikra ambao msomaji anaupata punde

anapolinganisha jina la ‘Kusadikika - Nchi iliyo Angani’ dhidi ya maelezo yanayoifafanua, “...ni nchi ambayo kuwako kwake hufikirika mawazoni tu...”. Huu ni ufutuhi fiche. Maelezo hayo ya mipaka yanaweza kuzua ucheshi kwa sababu ya kuwa nje ya uhalisi, hivyo kumsababishia msomaji pengo baina ya maana ya msingi na ile ya kimuktadha atakayoipata.

Hali ya pande za Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi kupakana na pepo za Kaskazi, Kusi, Matlai na Umande mtawalia huleta ugumu kwa msomaji kupata picha halisi ya jinsi pepo hizo zinavyoweza kusimama kama mipaka. Katika hali ya kawaida, daima pepo huwa katika hali ya mwendo. Huweza kuwa mwendo unaotokana na mfumo fulani ambao ni maalumu au ule unaotokana na sababu nyingine za kifizikia au kijiografia zinazobadilika mara kwa mara. Ni vigumu sana kwa pepo kuwa katika hali tuli. Hivyo, hata mkondo ambao unaunda ukanda fulani wa pepo mara nyingi huhamahama. Kutokana na uelewa unaopatikana kutoka katika maana hii ya msingi, msomaji ataweza kujiuliza juu ya uyakini wa mipaka hiyo. Suala kama hili ndilo linaloweza kuzua ucheshi kutokana na ufutuhi huu.

Kwa kutumia dhana ya utukuzaji ambayo imeongoza kupata maana ya kimuktadha ya tukio hili, tunaamini kwamba mtunzi anaizungumzia mojawapo ya nchi au jamii iliyopo katika ulimwengu halisi. Dhana ya mipaka ameitumia ili kudhihirisha kuwa nchi hiyo haiko kwenye ombwe. Kimuktadha, pepo nne zinazoizunguka nchi hiyo zinazitaja nchi halisi. Ithibati ya kwamba Robert anaitaja nchi halisi ni uhalisi wa maudhui ya kazi yenyewe.

Mipaka ya nchi hiyo ya Kusadikika ikimakinikiwa na msomaji kwa jicho la kihemenitiki, kupitia ukisiaji, inampatia maana mbalimbali. Upande wa Mashariki inapakana na pepo za Matlai. Matlai ni mkondo wa upepo ambao, aghalabu, huvuma kutoka baharini (TUKI, 2004). Hivyo, hapa Robert anatuambia kuwa nchi anayoitaja, kwa upande wa Mashariki imepakana na bahari. Kwa upande wa Magharibi, inapakana na pepo za Umande. Umande ni mvuke uliopoa na kugeuka maji, kisha kutua juu ya uso wa ardhi. Mvuke huo hutokana na mkondo wa hewa-joto kukabiliana na kitu au eneo lenye mkondo baridi. Katika muktadha huu wa kijiografia, kitu au eneo hilo husimama kama kizuizi cha kuvuma kwa mkondo-joto huo. Hivyo, hugeuka kuwa maji ambayo hutua chini kama manyunyu madogomadogo sana. Aghalabu, umande huweza kudhihirika bayana katika majani. Maelezo haya yanatuleta katika kusadiki kuwa Magharibi

mwa Kusadikika kuna milima au miinuko au miti ambayo huzizuia pepo za Matlai zenye joto kutoka baharini na kuzifanya zigeuke umande. Upane wa Kaskazini imepakana na upepo wa Kaskazi, na kwa upande wa Kusini imepakana na upepo wa Kusi.

Nchi ya Tanganyika (sasa Tanzania) inakidhi sifa hizi za kimipaka, kwamba Mashariki kuna bahari na Magharibi kuna miinuko. Pia, Kaskazini mwake hupokea pepo za Kaskazi zinazotoka katika pembe ya Afrika, na Kusini hupokea pepo za Kusi zinazovuma kutokana na mkondo-joto wa Msumbiji. Hivyo, hapa Robert anaizungumzia Tanganyika kwa kutumia fumbo hilo zito la kuifanya nchi hiyo iwe inaelea. Huu ni ufutuhi kwa kuwa msomaji anapobaini maana hii ya kimuktadha juu ya mipaka anayoisema mtunzi anaweza kuingiwa na furaha. Kwa jicho la kisilaha, usanaji huu wa madhari ya kifutuhi una uwezo mkubwa wa kuchengesa au kusahaulisha kiini cha jambo halisi linalozungumziwa.

Kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Uhemnitiki, maudhui ya *Kusadikika* yanatosha kuelezea sababu za mtunzi kuizungumzia nchi yake kwa kutumia fumbo hili. Riwaya hii iliingizwa katika mashindano ya utungaji wa vitabu vya Kiswahili mwaka 1948. Robert alikuwa mshindi wa kwanza katika shindano hilo ambalo liliandaliwa na chama cha kustawisha lugha ya Kiswahili, Afrika Mashariki. Nguvu ya kimamlaka ya chama hicho ilikuwa mikononi mwa Waingereza. Si shabaha ya makala hii kujishughulisha na kujua iwapo Robert alitunga mahsusi ili kuingiza kwenye mashindano tu au kwa lengo la kutaka watu waisome kama kazi nyingine za fasihi. Jambo la muhimu ni kwamba, vyovyote iwayo, kazi hii ilitungwa wakati wa ukoloni. Hivyo, vipengele vya fani na maudhui yake lazima vifungamane na hali hiyo ya ukoloni.

Majivuno, ambaye jina lake linabeba sifa hasi, ndiye Waziri Mkuu wa nchi ya Kusadikika. Yeye ndiye mtendaji mkuu wa shughuli za serikali. Kimamlaka, juu yake yupo mtu mmoja tu ambaye ni Mfalme. Pamoja na jina hilo kudokeza sifa hasi, mtunzi anampamba kwa sifa ya kwamba ni “mtu mwenye haiba kubwa na uhodari mwingi” (uk. 1); na kwamba, sifa hii ndiyo inayosababisha aitwe Majivuno. Hii ni kejeli ya wazi. Majivuno, siyo tu ana jina lenye sifa hasi, bali pia anamiliki sifa mbaya kama mtunzi mwenyewe anavyotuambia kwamba “... alijaa tadi na inda” (uk. 1). Tadi ni wivu, na inda ni kinyongo; hivyo Majivuno alikuwa mwivu na aliyekuwa anatomia uwezo wake kuwadidimiza wote waliojichomoza kwa lolote zuri kutokana na

kinyongo chake. Sifa hizo za Majivuno zinabainishwa kupitia maneno yake yaliyojaa dharau anaposoma mashtaka ya Karama asemapo, “Weusi wa nywele za mshtakiwa waonyesha waziwazi ujinga alionao” (uk.10). Katika nukuu hizo zote, Robert anazipiga kijembe kikali serikali za kikoloni kwa kuwaweka madarakani watu ambao walikuwa na sifa zisizostahili. Kutokana na uhalisi wa maana ya jina, pamoja na tabia za mwenye jina, jina hili linaponasibishwa kwa sifa za uhodari na u-jalali, kama anavyofanya mtunzi, hali ya ucheshi inaweza kuchipuka miongoni mwa hadhira.

Majina ya viongozi wengine wa serikali ya Kusadikika (Taadabuni, Katibu wa Serikali, Bwana Komeni, Amiri Jeshi, Bwana Fujo, Mlinda Hazina, na Bwana Boramimi, Mudir wa Sheria) nayo yanaweza kuzua ufutuhi. Ufutuhi wa Robert katika majina haya unajidhihirisha kupitia uteuzi wa majina ya kifutuhi yanayopingana na madaraka yao. Jeshi ni asasi yenye mamlaka ya kuilinda nchi na wananchi kwa kutumia hazina yote ya silaha za nchi husika. Viongozi wa asasi hii wanatakiwa kuwa waadilifu, wapole na wenye busara. Jina la Komeni linabeba sifa zilizo kinyume na hizo. Hii inaonesha kwamba ilikuwa rahisi kwake kutumia silaha za Wasadikika kuwanyanyasa na kuwanyamazisha wale wote wanaoibua hoja na malalamiko dhidi ya serikali. Idara ya fedha ndiyo kiini cha uchumi wa nchi; hivyo inafaa isimamiwe na watu walio makini katika kutunza mapato na kupanga matumizi yote. Jina la kiongozi wa idara hii katika nchi ya Kusadikika, Fujo, linamaanisha kuwa alikuwa mtu wa mipangilio na matumizi ya hovyohovyoy. Pia, asasi ya sheria inafaa iendeshwe na watu wenye uadilifu. Mudiri wa asasi hiyo katika nchi ya Kusadikika ni Boramimi. Jina hili linabainisha kwamba sheria za Kusadidika ziliweza kupindishwa wakati wowote kwa lengo la kumnufaisha Mudiri huyo au viongozi wengine. Bila shaka, upindishaji huo ndio uliosababisha Karama aanzishe darasa la kuwafundisha Wasadikika elimu ya sheria ili kuwakomboa dhidi ya ubinafsi huo wa Boramimi ambao anaubainisha hata katika kuifasili elimu ya uanasheria anapopindisha ukweli kwa kutuambia kwamba, “Uanasheria ni elimu ya kupingana na sheria” (uk. 8).

Robert, kupitia ufutuhi, anatuambia kuwa nchi ya Kusadikika ilikuwa na matatizo kama vile ufujaji wa mali, kujitenga dhidi ya nchi nyingine, kukosekana kwa uhuru na amani, na kutofanya mambo kwa kiasi. Matatizo hayo yanahusiana sana na majina hayo ya kifutuhi. Fujo ndiye

anayesababisha kupotea kwa fedha na uchumi wa Kusadikika. Akizungumzia kuhusu ubadhirifu, Robert anasema:

Watu watumiao mali zao kwa ubadhirifu husemwa kuwa wametumbukia katika maangamizi ya matumizi. Mwisho wa watu hao huvunjwawunjwa katika maanguko ya umaskini, yaani, njaa, kiu na uchumi. Watu watumiao mali zao kwa uangalifu huyaepa maanguko ya umaskini (uk. 32).

Nukuu hii inahusu matunda ya mjumbe wa Magharibi, Auni, ambaye aliiletea Kusadikika. Robert anaionya jamii kuhusu madhara ya ubadhirifu.

Komeni, kwa upande wake, ndiye chanzo cha kukosekana kwa amani nchini Kusadikika. Mtunzi anamtumia Fadhili, mjumbe wa Mashariki, kuhubiri umuhimu wa amani kwa kutuambia: “Neno uadui na mengine mabaya kama yajulikanavyo, watu walikusudia kujaribu kuyatoa katika lugha na kuyafuta katika vitabu”, (uk.18). Vilevile, Boramimi na Majivuno ndio waliosababisha kukosekana kwa utawala wa kisheria ambao unawafunga raia wa nchi hiyo wasio na hatia. Huu ni ukosefu wa huruma. Pia, ni matokeo ya matumizi ya madaraka yaliyopitiliza kiwango cha kawaida. Katika kutatua tatizo hili, Robert anamtumia Ridhaa, mjumbe wa Mbinguni, kuwaelimisha walimwengu kuhusu umuhimu wa kutenda wema na kuoneana huruma.

Kwa jumla, mtunzi ametumia ufutuhi kuiumbua serikali ya Kusadikika ambayo ndiyo chanzo cha matatizo yanayoikumba nchi hiyo. Ni vigumu kupata majibu, katika uhalisi wa mambo, kuwa iweje baraza la mawaziri likaongozwa na mtu mwenye sifa mbaya kama Majivuno? Iweje, idara ya fedha ambayo ni nyeti iongozwe na mtu asiye na maadili ya utunza hazina kama Fujo? Kwa nini idara ya sheria ambayo ndiyo mhimili wa haki za raia iongozwe na mtu mbinafsi kama Boramimi? Pia, kwa nini shughuli muhimu ya ukatibu wa serikali ifanywe na Taadabuni? Haya ni miongoni mwa maswali yajengayo ufutuhi kutokana na majina hayo. Robert anashadidia kejeli yake kwa serikali ya Kusadikika anapowaita watu hao kuwa ni “watu walio maarufu na waliipatia sifa Kusadikika” (uk. 5). Sifa anayoisema hapa ni kijembe kilichojaa unyume ambacho kilikusudia kuikeketa serikali hiyo. Hii ni kwa sababu Kusadikika inasawiriwa ikiwa imekithiri matatizo katika kila sekta. Zaidi, anafumba fumbo zito kuhusu uhusiano uliopo baina ya chanzo cha matatizo ya nchi ya Kusadikika, majina ya viongozi wa serikali, pamoja na

masuluhisho ya matatizo hayo ambayo yamefungiliwa katika maudhui ambayo kila mjumbe alirudi nayo kutoka katika safari yake.

Ufutuhi mwingine ambao Shaaban Robert ameuunda kupitia mbinu hii ya majazi ni wa kimgongano. Mgongano huo unahusisha wahusika wenye majina yenye ufutuhi. Huu hauishii tu katika maana na dhima za wahusika hao, bali huzipambanisha pande mbili zenye majina yenye sifa zinazokinzana. Upane mmoja yupo Karama ambaye anawawakilisha Auni, Buruhani, Kabuli, Fadhili, Amini, na Ridhaa. Upane wa pili yupo Majivuno ambaye anawawakilisha Fujo, Boramimi, Taadabuni, na Komeni. Upane wa raia unaoongozwa na Karama una majina yenye sifa chanya, wakati ule wa serikali unaoongozwa na Majivuno una majina yenye sifa hasi. Hivyo, ni rahisi kuzua ufutuhi pale mtu anapoyalinganisha na dhima na dhamana walizokabidhiwa serikalini. Huu ni ufutuhi fiche ambao unahitaji mtu azamie kwa kina ili kubaini kile ambacho Shaaban amekusudia kutokana na ukinzani baina ya makundi haya. Mwisho, kupitia utetezi wa Karama ambao ulileta ukombozi wa Kusadikika, Robert anatuonesha kwamba mrengo chanya uliushinda mrengo hasi.

3.2.2 Ufutuhi wa Unyume

Imekwishaelezwa katika utangulizi wa makala hii kuwa ufutuhi hutokea kwa kutegemea mojawapo ya namna mbili—kuwapo kwa ridhiko la nafsi kutokana na mvuto uliodhihirishwa au kuwapo kwa pengo. Msingi wa kuibuliwa kwa ufutuhi wa unyume ni kuwapo kwa pengo. Tukio la kwanza lenye ufutuhi wa unyume katika riwaya ya *Kusadikika* ni hili ambalo Robert analitoa kupitia kinywa cha kiongozi mmojawapo wa serikali ya nchi ya Kusadikika:

Mshtakiwa ana maneno mengi kama kitabu. Nakanusha kuwa anajua kitu chochote juu ya hekima. Hekima ni kitu adimu kupatikana na mtu asiye mvi. Weusi wa nywele za mshtakiwa waonyesha waziwazi ujinga alionao (uk. 9-10).

Nukuu hii inawasilisha majigambo ya Majivuno, Waziri Mkuu wa Kusadikika, ambayo anayatoa wakati anasoma mashtaka juu ya mhusika mkuu wa riwaya hii, Karama. Mtunzi hapa ametumia taswira ya rangi ya nywele kuufungulia ufutuhi wake. Hii ni namna maarufu ya kufanyiana utani katika fasihi nenwa. Katika maisha ya kila siku, binadamu hufanyiana ufutuhi kwa kuelekeza

katika sehemu mbalimbali za mwili, hususani usoni na katikati ya mwili, pamoja na michakato ambayo inafanywa na sehemu hizo, au matokeo yanayotokana na michakato hiyo.

Katika tukio hili, mtunzi amejiegemeza katika hali hiyo ya kijadi katika kuujenga unyume. Anaturejesha katika zama ambazo ustaarabu na fikra za Waafrika haukuwa chochote mbele ya ustaarabu na fikra za wakoloni. Anaturejesha pia kwa njia ya utani katika zama ambazo weupe wa nywele ulikuwa kipimo cha busara na elimu. Ucheshi wa wazi, kama zao la ufutuhi huo, unajitokeza msomaji asomapo Karama akimsimanga Majivuno waziwazi kwa kumwambia: “Elimu ilipokuwa haijulikani duniani, mvi zilihesabiwa kuwa alama ya hekima. Fikira hii ilikuwa njema sana, lakini wakati wake umepita wala haurudi tena. Sasa kama mtu hakuelimishwa, mvi zake hazihesabiwi kuwa dalili ya hekima” (uk. 10).

Pia, kupitia kejeli nzito, mtunzi anatuonesha jinsi wananchi walivyokuwa wanadhulumiwa haki zao. Kuhusu hili, Robert anasema:

Sheria za Kusadikika zilikuwa hazimwamuru mshtakiwa kujitetea juu ya ushahidi wa mshtaki. Aghalabu, mashtaka mengi yalikubaliwa bila ya swali wala kiapo. Labda ndiyo sababu ya nchi yao kuitwa Kusadikika (uk. 7).

Nukuu hii inabainisha jinsi Wasadikika walivyokuwa wananyanyaswa na mfumo wa sheria za nchi yao.

Utii, ambao nguzo-msingi yake ni kusadiki ni jambo ambalo watu hupenda kuliona likidhihiri kwa watu wanaowahusu. Mzazi kwa mwanawe, mwalimu kwa mwanafunzi wake, na viongozi kwa waongozwa, wote hutamani kutiwa na kusadikiwa. Hata hivyo, sifa hii anayoitoa Robert juu ya Wasadikika kuzitii sheria za nchi yao ni hasi. Mtunzi katika tukio hilo anawapumbaza walengwa wa kejeli hii kwa kuusifia uanakondoo wa Wasadikika, huku kwa sura ya ndani, akitumia kijembe kikali kuwakeketa kwa uyabisi wa sheria zao ambazo haziwapi watuhumiwa uhuru wa kujitetea.

Tukio lingine lenye maudhui yanayowasilishwa kwa kutumia ufutuhi wa unyume katika riwaya hii linagusia vipengele muhimu vya ustawi wa jamii. Robert anasema:

Kwa habari za miji mikubwa, ilisemwa kuwa vibanda katika vijiji mbalimbali (vya nchi ya Kusadikika) vikikusanywa pamoja vitatosha kuwa miji mikubwa. Juu ya majengo ya aushi, ilihesabiwa kuwa maisha ya mtu ni mafupi, kwa hivi, majengo ya aushi yalikuwa kazi ya bure. Kwa kuwa unyayo wa mtu hauzidi urefu wa inchi kumi na mbili wala upana wa inchi sita, ilifikiriwa kwamba ilikuwa ni hasara tupu kutengeneza barabara na daraja. Njia yoyote ya desturi ilitosha kwa safari za mtu. Maradhi yalidhaniwa kuwa kama matokeo ya kuja na kuondoka yenyewe bila ya msaada wa tabibu. Ukulima ulionekana hauna haja ya kusitawishwa wala kuhifadhiwa; na kuwa mfugaji mwema hasiti kushirikiana nyumba moja na wanyama wake (uk. 14, ufafanuzi wa kwenye mabano ni wa mwandishi wa makala hii).

Nukuu hii inawasilisha majibu ya serikali ya Kusadikika dhidi ya matunda aliyoyaleta Buruhani, mjumbe aliyejitolea kwenda upande wa Kaskazini. Mambo yaliyobebwa katika ujumbe huu ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii yoyote, hususani zile zilizokuwa chini ya makucha ya wakoloni kama ilivyokuwa Tanganyika. Robert hapa alikuwa anaumulika mchakato wa kimaendeleo ambao unahusisha hatua mbalimbali zinazopaswa kufuatwa na serikali. Hatua hizo ni kufuatwa kwa mbinu bora za kilimo cha uzalishaji wa mazao na mifugo, kuwapo kwa miundombinu imara kwa ajili ya kusafirishia mazao ya kilimo, pamoja na kuimarishwa kwa sekta ya utabibu ili kuwa na watu wenye afya njema ambayo itawawezesha kufanya kazi za maendeleo. Vilevile, ujumbe ulisisitiza uboreshaji wa miji yetu. Haya ni masuala mazito yaliyokuwa akilini mwa Robert, na ambayo alitaka ayafikishe kwa umma.

Msomaji akitaka kujua uzito wa masuala haya, ni vyema, kwa kuzingatia mhimili wa ufufuaji wa Nadharia ya Uhemnitiki, akarejesha akili yake juu ya kiwango cha maendeleo ya wakati huo kwa kujiuliza maswali yafuatayo: Kilimo cha mazao na ufugaji wa wanyama kilikuwa kinaendeshwaje? Kilikuwa na ufanisi gani kwa wakulima wenyewe? Miundombinu kama vile madaraja na barabara ilikuwa katika hali gani? Hali ya huduma za kitabibu kwa Watanganyika ilikuwaje? Robert alikuwa amekwishaathiriwa na madhila yaliyotokana na mengi ya mambo yanayododoswa kupitia maswali hayo. Mulokozi (2002) anabainisha kuwa, katika wakati huohuo, kupitia barua alizokuwa anamwandikia mdogo wake (Yusufu Ulenge), mtunzi alikuwa anatoa taarifa za mara kwa mara kuhusu vifo vya mapema vilivyokuwa vinawapata watoto wake wachanga. Yamkini, hali hiyo ilitokana na kukosekana kwa huduma bora za afya. Pia, tawasifu ya mtunzi (Robert, 1966) inatuonesha kuwa, ni katika wakati huohuo alikuwa anapatwa na matatizo yanayotokana na uduni wa njia za usafiri. Kwa mfano, tawasifu hiyo inatuonesha

kwamba (Robert) alishindwa kuusafirisha mwili wa marehemu mkewe, Amina, kutoka Wilaya ya Pangani hadi kijijini kwake, Vibambani, (Wilaya ya Tanga) kwa ajili ya maziko kutokana na barabara kuharibiwa na mvua. Hivyo, nukuu ya hapo juu ni kijembe kingine kikali kwa viongozi wa serikali za kikoloni.

Ufutuhi katika tukio hilo lililodondolewa kutoka ukurasa wa 14 uko wazi kwa sababu ya unyume wa hoja zenyewe. Hoja hizo za serikali zenye ufinyu wa kifikra zinapingana kwa wazi na mawazo nyumbufu ya Robert yaliyomulika hali ya maisha ya jamii yake kwa kipindi cha miongo kadhaa ambayo ingefuatia kutoka muda wa utunzi wa kazi hiyo. Akiwa mmojawapo wa waathirika wa uduni wa huduma za jamii zilizokuwa zinasambazwa wakati huo kwa wananchi, yamkini Robert alikerwa na jinsi wakoloni walivyokuwa wanapuuzia suala hilo. Akaamua kupambana nao kwa silaha hii ya vijembe na mafumbo ambayo yalibeba ufutuhi.

Fikra nyingine ya Robert katika *Kusadikika* imo katika tukio lenye ufutuhi wa unyume linalowahusisha wahusika Sapa na Salihi. Anasema:

Bwana wangu mwema, mimi naitwa Sapa na mwenzangu ni Salihi. Salihi haombi neno akalikosa. Ameishi maisha haya tangu ujana wake, lakini vitu alivyovipata kwa maombi aliyoyafanya alikuwa hana matumizi navyo. Nilipoona hivyo nilimwambia kuwa niliota ndoto kuwa akiomba kitu chochote tena bila ya kugawana na mimi sawasawa, dua lake halitapokewa hata kidogo. Kwa sababu hii, tuliafikiana kushirikiana kila kitu atakachokiomba tukaandikiana hati mbele ya kadhi. Hati ya mkataba wetu ilipokwisha kuandikwa nilifurahi sana kuwa shauri langu limefaulu, lakini pale pale mwenzangu aliinua mikono yake juu akaomba upofu, na kabla sijatanabahi, sisi sote wawili tulikuwa vipofu (uk. 29 - 30).

Kwa mara nyingine, viungo vya mwili wa binadamu (uso) vinatumiwa katika kutengeneza ufutuhi. Waswahili wana kaida ya kuunda au kuelekeza mafumbo, kejeli, dhihaka, utani na vijembe vingi katika pua, masikio, mashavu, macho, midomo, au uso wote kwa jumla. Katika tukio hili, mtunzi ameonesha kuwa karibu sana na jadi hii. Anatomia kiungo cha macho kuviringishia wazo lake la athari za wivu. Matarajio ya Sapa yanaonekana kuwa kinyume na mawazo ya Salihi kama anavyotumbia:

Mimi naapa kuwa sikujua kama Sapa alitamani ufalme au utajiri wakati aliponiagulia ndoto yake. Laiti ningalijua nia yake ilivyokuwa, hili lisingalitokea.

Ningaliomba madua mawili mbalimbali yaani, moja langu na jingine lake na kila mmoja katika sisi angalipata haja yake. Nilipoona mambo ya dunia yamenichukiza, nilidhani kuwa na mwenzangu yamemchukiza vilevile, na kwa mujibu wa mapatano yetu nikaomba upofu ili tuishi bila ya kuyaona tena. Madhali neno nililoliomba nimelipata, wajibu wangu sasa ni kushukuru. Haiwezekani kuomba niyaone tena mambo niliyoyakataa (uk. 31).

Kwa mara nyingine, katika nukuu hii mtunzi amenyunyizia majazi katika kujenga ufutuhi wa tukio hili unaoweza kujidhihirisha kwa wazi. Sapa, ambaye maana yake ya msingi ni kufilisi au kuchukua kitu au mali yoye ya mtu bila ya kumbakizia, amejengwa akiwa na nia ya kumfilisi Salihi, ambaye jina lake linatupa picha ya mtu anayesali na kumcha Mungu. Ufutuhi huo umejikita katika tofauti inayojitokeza baina ya matarajio aliyokuwa nayo Sapa na mawazo aliyokuwa nayo Salihi, ambayo yanamletea Sapa matokeo yaliyo kinyume na matarajio yake. Kwa kutumia msingi wa ufufuaji, tukio hili la Sapa na Sahili linaweza kuhusishwa na wivu, ulafi, na usapaji uliokuwa unafanywa na wakoloni dhidi ya malighafi za Watanganyika na Waafrika kwa ujumla. Hivyo, kwa kutumia fikra hizo za kihemenitiki, inajuzu kusema kuwa maudhui haya yalikuwa yanawang'ong'a wakoloni juu ya u-sapa wao.

3.2.3 Ufutuhi wa Balagha

Kwa mujibu wa Ponera (2014), balagha ni ukuzaji wa jambo au utiaji wa chumvi katika jambo. Jambo huweza kutendwa au kusimuliwa kwa kupitiliza katika ukawaida au uhalisi wake. Balagha ni kipengele maarufu katika matumizi ya lugha ya masimulizi. Watumiaji wa lugha ya mazungumzo mara nyingi hukitumia kipengele hiki katika mazungumzo yao ya kawaida.

Riwaya ya *Kusadikika* ina matukio yenye ujumbe mzito ambayo Robert ameyawasilisha kwa kutumia ufutuhi wa balagha. Tukio la kwanza linahusu sifa za uzazi kwa wanawake wa nchi ya Kusadikika. Robert anasema:

Wanawake wote katika nchi hiyo huzaa watoto pacha. Hii ni habari ya ajabu sana lakini haionekani kuwa imepata kugusa ndoto za wazee. Wasimulizi bado kuisimulia, wala haijawashawishi wapima kuitia nchi hiyo katika ramani, (utangulizi).

Kwa hakika, hakuna jamii yenye sifa hii ya uzazi duniani kote. Hata hivyo, ni wazi kuwa mtunzi anaizungumzia jamii mojawapo ya hapa duniani. Uzazi anaouzungumzia hapa ni jazanda ya

neema zilizojaa nchini Kusadikika. Neema hizo amezihusisha kuwa zinatokana na wanawake ili kuufanikisha msimamo wake juu sifa na hadhi ya wanawake katika jamii. Tulibaini kuwa sababu iliyomsukuma mtunzi kuitumia balagha hii ni kuwapumbaza wenye fikra nyepesi katika kutafakari, huku kwa upande mwingine, akijitanibu na wale waliokuwa na uwezo wa kutafakari na kuuvumbua ukweli uliopo katika riwaya hii.

Balagha nyingine ya Robert tunaiona katika tukio linalohusisha fikra za kimajazi. Tukio hilo linamhusisha Mfalme Jeta. Anasema:

Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta, alimkuta amekaa kitako midomo wazi. Mto mrefu na mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana. Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukiepa kinywa hicho. Tani milioni moja za mwamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo, na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani pia kila dakika tano. Lakini kila dakika moja Jeta alilia: ‘Kiu, njaa, kiu, njaa!’ (uk. 23 - 24).

Nukuu hii ina ufutuhi wa wazi. Hili ni mojawapo ya matukio yaoneshayo kilele chake cha matumizi ya mbinu hii ya balagha katika kuwasilisha mambo. Balagha hii haiishii tu katika kutudokezea hali ya ulafi wa viongozi wetu, bali ina zaidi ya hayo. Imekwishaelezwa katika sehemu zilizotangulia za makala hii kuwa miongoni mwa maana za neno ‘jeta’ ni ‘mtu mvivu apendaye kuwatuma wenzake wamletee vitu ijapokuwa viko karibu naye’ au ‘kufanya maringo kwa kitu ulichonacho; kujivuna’. Kabuli, mjumbe wa Kusini anakutwa na masaibu haya akiwa katika nchi ya Juju. Juju ni uchawi. Aghalabu, uchawi hunasibishwa sana na matukio ya ukatili. Hivyo, wana-Juju wamechorwa kuwa na ukatili uliokithiri. Kupitia nukuu hii, Robert anaidokeza hadhira yake kuhusu ulafi, uroho, ujivuni, uvivu, na ukatili wa mtu mmoja mmoja hadi wa kitaifa. Maoni ya makala hii ni kwamba, kama ilivyokwishadokezwa kuhusu mipaka ya Kusadikika, mashambulizi ya Robert katika tukio hilo, mbali na kuwalenga wakoloni wa Tanganyika, pia yameelekezwa kwa makaburu wa Afrika Kusini. Nchi ya Afrika Kusini, kama ilivyokuwa kwa Tanganyika, ilisheheni kila aina ya utajiri, hususani wa madini na misitu, ambayo mtunzi analalamika katika tukio hilo kwamba ilikuwa inaporwa na walafi, waroho, wakatili, wavivu, na wajivuni hao.

Kutokana na balagha iliyomo kwenye nukuu hiyo, yenye dhihaka na fumbo, nani angeweza kumnyooshea kidole cha ole juu ya sifa mbaya hizo alizozitongoa kuhusu majeta hao? Tunaamini kuwa wakoloni wengi waliolisoma tukio hili waliishia ‘kusahaulishwa’ au ‘kupumbazwa’ na ufutuhi. Yumkini, hata wachache ambao walivuka hapo na kujiuliza maswali kama vile ‘ulafi wa nani?’, ‘ulafi wa nini?’, na ‘ulafi wa lini?’ hawakuwa na ithibati za wazi ili kumnyooshea kidole cha ole au kumwadhibu. Majuju wanaosawiriwa na Robert kwa wakati huo walikuwa makaburu na wakoloni wengine ambao walizivamia nchi zisizo zao kwa ajili ya kupora mali na kuwanyanyasa wenyeji wao. Pia, kwa wakati huu, hususani katika nchi zetu zinazoendelea, majeta ni watu wote wenye nguvu za kimamlaka katika asasi, taasisi, na serikali kwa ujumla ambao tabia zao za kinadharia au kimatendo zinasadifu u-juju na u-jeta². Balagha hiyo inamalizika kwa kuoneshwa namna Kabuli alivyookoka kiajabu kutoka katika zahama hizo za u-juju na u-jeta. Tunaambiwa:

Kabuli alipokuwa anachimba kaburi lake kwa kisigirima, ilichimbuka johari kubwa na nzuri sana ... Adhabu yake ya kwanza ilipokwisha, alitoka nje akawaonyesha askari waliokuwa wakimlinda johari aliyoigundua. Kwa kuona hivi, kila askari alidai johari ile kuwa yake. Palepale lilitokea pigano kati yao lililowasukuma wote wawili hatika kaburi lililokuwa wazi, wakatumbukia ndani yake kwa mshindo mkubwa sana. Mshindo huu uliufanya mchanga wa pande zote nne juu ya kaburi kubomoka na kuwaelekea juu yao. Walikufa wakati uleule. Kwa tokeo hili, Kabuli aliokoka pamoja na johari yake (uk. 24 - 25).

Matukio ya wokovu huu yamekolezwa sana, hayana uhalisi. Kinachoonekana hapa ni namna ambavyo Shaaban alizoea na kuingiwa na matumizi ya balagha katika utunzi wake.

3.2.4 Ufutuhi wa Utanakuzi

Utanakuzi ni hali ya kukinza dhana mbili zenye sifa tofauti. Aghalabu, kila moja ya dhana hizo huwa na maana iliyo kinyume na nyingine (Wamitila, 2003). Umilisi wa kutosha wa lugha ndiyo nyenzo muhimu inayoweza kumsaidia mtumia lugha kutengeneza utanakuzi. Lugha ya

²Kazi hii ya *Kusadikika* inafaa sana kusomwa na viongozi wa leo katika nchi zetu za Afrika, au wasomewe ili waelewe. Ni kazi yenye matukio ambayo yana uhai kwa wakati huo, wa sasa, na ujao. Shaaban Robert, katika suala hili hachekeshi tu, bali anawacheka na kuwasema viongozi wetu ambao ni majeta kutokana na uovu mwingi—kama vile ubadhirifu, kujilimbikizia mali, utegevu, na uonevu—ambao wanaufanya kwa kutumia nafasi zao (Prof. Mgyabusu Mulokozi, mazungumzo na mwandishi wa makala hii yaliyofanyika tarehe 30/09/2009).

kitanakuzi husababisha hadhira kupata utamu, hususani, pale hadhira hiyo inapokuwa na kiasi cha kutosha cha umilisi wa lugha iliyotumika. Wakati mwingine, utanakuzi hutumika kutengenezea balagha, kejeli, dhihaka au mafumbo. Hivyo, tungo ya kitanakuzi ibebapo vipengele hivi ndipo huhusishwa na ufutuhi; kwamba, huwa utanakuzi wa kifutuhi. Hii ni kwa sababu huwa na uwezo wa kusababisha hali za kicheko, ucheshi au furaha kwa anayesoma au anayesikiliza kutokana na mnato wa lugha. Vitanza-ndimi na vichezea-maneno vingi vya lugha ya Kiswahili ni sehemu ya mifano ya matumizi ya utanakuzi.

Zaidi ya ufutuhi fiche wa kuelimisha na kuuzindua umma alioutumia katika *Kusadikika*, Robert anajitokeza pia katika riwaya hii kucheza maneno ili kupata ufutuhi kwa ajili ya kuwafurahisha wasomaji wake. Ufutuhi wa utanakuzi umejitokeza kwa kiasi kidogo sana katika riwaya teule. Tukio la kwanza la kitanakuzi ni hili lifuatalo:

Mtu yeyote anayeyapa mgongo, akayaonyesha visigino mashaka yanayostahili kushindwa—kama kuishinda njaa kwa kilimo, kiu kwa visima, mifereji, au mabomba; umaskini kwa kwa kazi; maradhi kwa utabibu ... Kama ni karaha kumlinganisha mwanadamu na mnyama au mdudu mwenye sifa mbaya, basi ni fahari pia mtu kulinganishwa na mnyama au mdudu mwenye sifa njema kama mchwa na wengine (uk. 29).

Katika nukuu hii, mtunzi anashadidia suala la walimwengu kujitahidi katika shughuli mbalimbali ili kujiletea ustawi. Ameliwasilisha jambo hili kwa kukinza dhana mbalimbali kwa namna ambayo inafurahisha. Halikadhalika, maudhui haya yakitazamwa kwa jicho la Duara ya Kihemenitiki inadhihirika kuwa Robert bado anaisawiri jamii yake iliyokuwa inakabiliwa na mikatale ya wakoloni.

Utanakuzi mwingine tunaupata katika kitushi cha safari ya Amini, mjumbe wa *Kusadikika* ambaye alikwenda huko Ardhini. Robert anasema: “Watu wa ardhi walinena kuwa maji yaliyo meupe kama theluji si maji ila theluji, na yaliyo mepesi kama hewa si maji ila hewa” (uk. 45). Katika tukio hili, Amini alishuku kuwa maji ya Ardhini yalikuwa yanatokana na damu ya Wasadikika iliyokuwa inapeperushwa na upepo na kudondokea Ardhini ikiwa nyeupe kama maji na nyepesi kama hewa. Licha ya maudhui yanayolizungukia tukio hili kutudokezea wazo chungu

la kukithiri kwa umwagaji wa damu ya Wasadikika wasio na hatia, pia linaweza kumfanya msomaji afurahi kutokana na mnato wa lugha iliyotumika.

Robert anaendelea kutongoa sifa kemkem kuhusu akili, juhudi na vipawa vya watu wa Ardhini kwa kutumia utanakuzi. Anasema: “Hawana mabawa, lakini huruka hewani kama ndege kwa vyombo. Hawana mapezi, lakini huzama baharini kama samaki kwa vyombo vilevile” (uk. 47). Anaongeza: “Kwa ubongo wao, hutunga na kutangua mambo mpaka wapate jambo la kufaa. Kwa kano zao, hujitwika na kujitua dhima kubwa na nzito (uk. 48). Matukio haya ni ithibati ya namna Robert alivyokuwa na uwezo mkubwa wa kuteua na kupangilia maneno. Sifa zote hizo anazitoa kwa kutumia mbinu ya kitanakuzi ambayo, mbali na kuwasilisha ujumbe alioukusudia kuhusu kuhamasisha matumizi ya teknolojia katika kuleta maendeleo, inasaidia kulainisha usomaji wa riwaya teule. Vilevile, wakati mwingine, msomaji anaposoma vipande vyenye utanakuzi anaweza kujikuta anaingiwa na furaha kutokana na usanii na ulainishaji huo.

4.0 Hitimisho

Makala hii imethibitisha kuwa mwandishi wa riwaya ya *Kusadikika* alipenyeza maudhui yake yenye mrengo wa kupambana na wakoloni kwa kutumia silaha ya ufutuhi. Pamoja na udhibiti mkubwa wa kazi za kifasihi uliokuwapo wakati huo, Robert alifanikiwa kutumia kipawa chake kushiriki vita vya ukombozi kwa kutumia kalamu yake. Makala imebainisha kuwa, kupitia riwaya ya *Kusadikika*, Robert anawashambulia wakoloni kwa kubeua na kung’ong’a sera na mifumo yao ya utawala. Zaidi, anaelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutumia elimu ili kujipapatua kutoka kwenye mazonge ya kikoloni. Yote haya ameyawasilisha kwa kutumia aina nne za ufutuhi ambazo ni: ufutuhi wa majazi, ufutuhi wa balagha, ufutuhi wa unyume, na ufutuhi wa utanakuzi. Ni wazi kuwa waandishi wa kazi za fasihi ni miongoni mwa makundi yanayotegemewa sana na jamii katika kuilea, kuiongoza, kuikosoa, na kuiokomboa. Hivyo, ni vyema waendeleo kuvaa ujasiri wa kufanya kazi yao kwa kutumia mbinu anuwai kama alivyofanya Robert kwa kutumia ufutuhi.

Marejeleo

Attardo, S. (2001). *Humorous Texts: A Semantic and Pragmatic Analysis*. Berlin and New York: Mouton de Gruyter.

- Billig, M. (2005). *Laughter and Ridicule: Towards a Social Critique of Humor*. London: Sage Publications.
- Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction*. Oxford: Basil Blackwell.
- Ebeling, G. (1964). The New Hermeneutics and the Early Luther, katika *Theology Today*, ya 21.1, 34-46. DOI: <https://doi.org/10.1177/004057366402100105>
- Kezilahabi, E. (1976). *Shaaban Robert: Mwandishi wa Riwaya* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam). Haijachapishwa.
- Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.
- Mulokozi, M.M. (2002). *Barua za Shaaban Robert (1931-1958)*. Dar es Salaam: TUKI.
- Newton, K.M. (1997). *Twentieth Century Literary Theory: A Reader* (2nd Ed.). London: Palgrave Macmillan.
- Ponera, A. S. (2014). *Ufutuhi katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma). Haijachapishwa.
- Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Nairobi: Nelson.
- Robert, S. (1966). *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Ross, A. (1998). *The Language of Humor*. New York: Routledge.
- Shitemi, N.L. (2008). Ushairi wa Jadi: Hifadhi na Kumbukumbu za Ustaarabu na Maendeleo ya Kimji Pwani ya Afrika Mashariki. *Kiswahili* (71/1), 36-48.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.